

## HITIMISHO

Mbuzi na kondoo ni wanyama wenye faida kubwa ukilinganisha na mahitaji yao. Mbuzi au kondoo huhitaji eneo dogo kuwafuga, mtaji mdogo na huweza kuchungwa sehemu ambazo kilimo cha mazao au ufugaji wa ng'ombe hauwezekani.

Wakifugwa kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu, wanyama hawa ni chanzo kizuri cha kipato.



## •Ufugaji bora na afya ya mbuzi na kondoo



Imetolewa na (Au kwa ushauri zaidi uliza;)  
Kliniki ya Mifugo  
Kitivo cha Tiba ya mifugo  
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo  
S. L. P. 3015  
Chuo Kikuu MOROGORO  
Simu: 0232 60 1495  
Fax: 023 260 4647

## **UTANGULIZI**

Kutokana na umbo lao dogo, mbuzi na kondoo ni rahisi kufuga kwani huhitaji eneo dogo, mahitaji yao ya chakula ni madogo ikilinganishwa na ng'ombe, na pia hupendelea majani ya miti ambayo ng'ombe hawali.

Siku hizi hapa Tanzania mbali na mbuzi wetu wa kienyeji, kuna mbuzi wa maziwa ambao wanaweza kumpatia mfugaji wastani wa lita 3—4 za maziwa kwa siku. Maziwa ya mbuzi ni matamu na hutumika kama dawa ya vidonda vya tumbo, Pia mbuzi hutupatia nyama, ngozi na mbolea.

Mbuzi wa maziwa hawastahimili magonjwa kama wale wa kienyeji na kwa hiyo wanahitaji matunzo na uanagalizi mzuri zaidi ili waweze kuzaa na kutoa maziwa mengi zaidi

## **UTUNZAJI**

### **NYUMBA**

Banda la mbuzi/kondoo linatakiwa liwe na nafasi, imara, safi, lenye hewa ya kutosha na sakafu kavu. Vumbi na baridi kali huwaathiri sana mbuzi/kondoo wadogo.

### **CHAKULA**

Mbuzi hula nyasi na majani ya miti aidha kwa kuchungwa au kukatiwa na kulishwa nyumbani. Chakula cha ziada chenye mchanganyiko wa pumba, mashudu na madini pia ni muhimu hasa kwa mbuzi wa maziwa. Pia mbuzi na kondoo wanahitaji maji safi ya kunywa.

## **KONDOO**

Mbuzi na kondoo hushambuliwa sana na magonjwa yafuatayo:-

- Minyoo
- Homa ya mapafu
- Kuoza kwato
- Viroboto
- Magonjwa ya ngozi (mange au ukuru)

Ili kuwakinga wanyama na matatizo haya mfugaji anashauriwa kufanya yafuatayo:-

- Kuwapa dawa ya kuua minyoo kulingana na ushauri wa wataalam wa mifugo wa eneo lako
- Kuhakikisha kuwa banda ni safi, sakafu ni kavu, isiyo na vumbi wala matope
- Kuwaoggesha wanyama kwa kutumia dawa inayoua wadudu waenezao magonjwa angalau mara moja kwa mwezi
- Kuwasiliana na wataalamu wa mifugo katika eneo lake mara tu ugonjwa unapotokea katika zizi lake.

## **MAGONJWA MUHIMU YA MBUZI NA**